

## **Kifo cha Irmu**

### *Bunduki Chihungi*

Kifo unampitia, aishiye duniani  
Hapana wa kukimbia, mbali usikofikia  
Watu wakifurahia, maisha watibulia  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifika**

Mchana unaingia, bila ya kusalimia  
Kifo usiku waingia, bila hodi kubishia  
Watu wakijilalia, kifo wawashambulia  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifia**

Kifo wawatishia, vijana wazee pia  
Matajiri wa India, na masikini sawia  
Katikati Tanzania, au hapa Austria  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifia**

Wafalme, Malkiam, kifo wajitwalia  
Hawawezi kukimbia, hodi ukiwapigia  
Mali wanazolalia, haziwezi saidia  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifia**

Augosti nakumbukia, mwaka huno 2011 waishia  
Irmu hukumwachia, aweze kujiishia  
Kwani ulimnuia, kwingineko kuhamia  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifia**

Habari kutufikia, Irmu umejifia  
Tulishindwa vumilia, huzuni kuzizuia  
Tukakujia kwa nia, mazishini kwa mamia  
**Irmu twakumbukia, mapema umejifia**

Chuo kikikumbukia, ni kama vile ruia:  
Umehama dunia, kifo nguvu kakuzidia  
Vitani uliingia, maisha kupigania  
**Irimi twakumbukia, mapema umejifia**

Tungalimshuhudia, kifo tungalimwambia  
Wewe kukuachilia, ufike miaka mia  
Chuo chakuhitajia, familia yako pia  
**Irimi twakumbukia, mapema umejifia**

Irimi nakuandikia, lugha ulojulia  
Chuoni kufundishia, Kiswahili asilia  
Na juu ukafikia, chuoni ukatumia  
**Irimi twakumbukia, mapema umejifia**

Irimi nakuambia, familia yako yalia  
Ertürk kawa mkiwa, nyuma alikobakia  
Watoto ajitunzia, huko uliko tulia!  
Na sala nakusalia, azipokee Jalia!!